10:1-36:23 WAFALME WA YUDA

Mgawanyo wa ufalme na matokeo yake (10:1-13:22)

Mwandishi wa Mambo ya Nyakati alieleza mgawanyo wa ufalme (10:1-11:4; taz. maelezo ya lFal 12:1-24), lakini hakutaja habari ya Yeroboamu kuwa mfalme wa kwanza wa makabila ya kaskazini iliyoandikwa katika lFal 12:20, wala hakutaja habari ya utawala wake wote wa makabila hayo (lFal 12:25-14:20). Yeye alifikiri kwamba makabila ya kaskazini, baada ya kujitenga na ufalme wa Daudi na kuacha ibada ya BWANA (YAHWEH), hayakuwa na haki ya kuitwa ufalme, na hasa siyo ufalme wa Israeli.

Kinyume cha mwandishi wa Wafalme (aliyeita ufalme wa kusini Yuda na ule wa kaskazini Israeli), mwandishi wa Mambo ya Nyakati aliita ufalme wa kusini Yuda au Israeli. Kwake yeye ufalme wa Yuda ni ufalme wa pekee ulio wa kweli, na wafalme wa nyumba ya Daudi ni wafalme wa pekee waliokuwa na haki ya kuitwa hivyo. Lakini aliendelea kuwakubali watu wa kaskazini kuwa Waisraeli, naye alifurahi baadhi yao waliporudi kwa BWANA (YAHWEH) na kwa watawala wa nyumba ya Daudi (taz.l 1:13-17; 15:9; 30:1-12). Mara nyingine aliutaja ufalme wa kaskazini kuwa Waefraimu.

Makuhani na Walawi walipata heshima katika maelezo ya Mambo ya Nyakati kuhusu maendeleo ya Yuda. Rehoboamu alianza utawala wake vizuri, hasa kwa sababu ya ushawishi wa idadi kubwa ya makuhani na Walawi waliohamia Yuda kutoka kaskazini, kuliko kujiunga na ibada ya sanamu ya Yeroboamu. Wakati wote Rehoboamu alipofuata njia ya BWANA kama alivyofundishwa na makuhani, Yuda ilikuwa imara na yenye nguvu. Alipoingiza mambo yaliyotokana na dini za Kikanaani, Mungu alimwadhibu kwa njia ya kushambuliwa na Wamisri walioharibu nchi (11:5-12:16; taz. maelezo ya lFal 14:21-31).

Ingawa Abiya alifuata siasa ya baba yake ya kuruhusu ibada ya Baali iendeshwe sambamba na ibada ya BWANA, hakumwacha Mungu kabisa kama Yeroboamu alivyofanya kaskazini. Ushindi wa Abiya juu ya Yeroboamu kwa jinsi asivyotazamia, ulionyesha kwamba Mungu alikuwa upande wa mfalme aliyekuwa wa nyumba ya Daudi ambaye pia alimwabudu BWANA (YAHWEH) (13:1-22; taz. maelezo ya lFal 15:1-8).

Marekebisho chini ya Asa (14:1-16:14)

Baraka ya Mungu juu ya Asa ilionyesha jinsi Mungu alivyopendezwa na wafalme wale walioondoa desturi za Kikanaani na kurekebisha mipango ya ibada ya Kilawi katika Israeli. Mungu aliheshimu bidii na imani ya Asa, akimpa ushindi wa ajabu juu ya jeshi kubwa na lenye nguvu lililokuwa limeshambulia Yuda kutoka kusini. Alama hiyo ya kibali cha Mungu ilimtia Asa moyo kuendelea na marekebisho yake kwa ushujaa zaidi (14:1-15:18; taz. maelezo ya lFal 15:9-15).

Ha Asa alipotegemea msaada wa kutoka nje kuliko kutegemea msaada wa Mungu, alimhuzunisha Mungu naye alikemewa na nabii mmojawapo. Asa hakutaka kusikiliza ushauri wowote, na hivyo alimtendea ukatili mtu ye yote aliyethubutu kupinga siasa yake (16:1-14; taz. maelezo ya lFal 15:16-24).

Karibu na mwisho wa utawala wa Asa, Ahabu alipata mamlaka kaskazini. Chini ya ushawishi wa mke wake wa kigeni, Yezebeli, Ahabu aliingiza aina mpya ya Ubaali katika Israeli. Ubaali huo ulikuwa na nguvu zaidi, nao ulikuwa mbaya sana kuliko ule ambao watu wa kawaida waliuzoea katika madhabahu za Baali au katika mahali pa juu sehemu mbalimbali nchini (lFal 15:25-21:29). Lakini mambo hayo yalihusu ufalme wa kaskazini, kwa hiyo mwandishi aliyefuata makusudi yake ya kawaida, hakuyaandika.

Utawala wa Yehoshafati (17:1-20:37)

Yehoshafati aliendelea na marekebisho ambayo baba yake alikuwa ameyaanzisha, akijaribu kubomoa madhabahu zote za Ubaali zilizobaki katika Yuda (17:1-6; taz. 15:17). Alifanya mipango ya kuwafundisha watu wote katika sheria ya Mungu, akituma kundi la walimu rasmi katika miji na vijiji vyote vya Yuda. Kundi lile lilikuwa na viongozi wa kiraia, makuhani na Walawi (17:7-9). Pia aliimarisha ulinzi wa Yuda na kuongeza jeshi lake, hata mataifa ya jirani yakaogopa kumshambulia (10-19).

Jeshi la Yuda lilikuwa na nguvu sana, hata Ahabu wa Israeli alitafuta na kupata msaada wa Yehoshafati katika vita vyake dhidi ya Washami (18:1-34; taz. maelezo ya lFal 22:1-40). Nabii mmoja akamkemea Yehoshafati kwa jambo hilo, kwa sababu Ahabu alimwabudu Baali, na hivyo alikuwa adui

wa Mungu (19:1-3).

Yehoshafati alisahihisha na kupanga upya kanuni yote ya mahakama katika Yuda, ili kuondoa mambo ya dhuluma na kuhakikisha hukumu ya haki kwa watu wote, na kuhakikisha kwamba mipango hiyo inatekelezwa nchini kote. Aliweka mahakama ndogo na mahakimu katika miji mikubwa yote ya Yuda, mahakama kuu ikaendelea kuwa Yerusalemu pamoja na mahakimu wake. Kulikuwa na aina mbili za mahakama na maafisa wake, yaani wale walioshughulika na mambo ya kidini wakiwa chini ya uangalizi wa kuhani mkuu; na wale walioshughulika na mambo ya kiraia wakiwa chini ya uangalizi wa Jemadari mkuu (4-11). Mipango hii ilikuwa alama nyingine kwa mwandishi wa Mambo ya Nyakati kwamba ufalme wa Daudi ulitawaliwa kadiri ya sheria ya Kilawi (taz.Kum 16:18-20; 17:8-12).

Baada ya muda jeshi kubwa la mwungano wa mataifa mbalimbali lilijipanga kushambulia Yuda kutokakusini na mashariki (20:1-2). Mwandishi wa Mambo ya Nyakati alieleza kwamba, licha ya Yehoshafati na watu wake kumlilia Mungu kwa msaada wake, walifanya hivyo wakikusanyika katika hekalu la Yerusalemu. Hapo palikuwa mahali rasmi pa maombi ya watu wa Mungu wakati wa shida (3-12; taz.6:24-25). Matokeo yake, Mungu alijibu maombi yao. Aliwahakikishia kwa njia ya nabii (ambaye pia alikuwa Mlawi) kwamba maadui wangeshindwa bila jeshi la Yehoshafati kufanya jambo lo lote (13-17).

Makuhani na Walawi waliokuwa na bidii sana katika Yuda wakati ule waliwaongoza watu katika nyimbo na sifa hata kabla ya ushindi wenyewe kupatikana (18-23). Baada ya watu kuteka nyara kwa maadui walioshindwa, waimbaji wa Kilawi waliwaongoza hekaluni ili kumsifu Mungu kwa ushindi wake mkubwa (24-30).

Kabla ya hayo, Yehoshafati alikuwa amekosa alipofanya mapatano ya kijeshi na Ahabu (taz.18:3; 19:2). Baadaye alikosa tena alipofanya mapatano ya kibiashara na mwana wa Ahabu, Ahazia. Mungu akatuma ajali kubwa ili kumwonya kwamba hakutakiwa kufanya mwungano na wafalme wa Israeli walioabudu Mabaali (20:31-37; taz. maelezo ya IFal 22:41-50). Mwandishi hakueleza mambo mengine ya utawala mfupi wa Ahazia yaliyoandikwa katika lFal 22:51-53.

Ubaali wa Yezebeli katika Yuda (21:1-23:21)

Ubaali wa Ahabu na mkewe Yezebeli uliendelea kuwa na nguvu katika ufalme wa kaskazini wakati wa utawala wa wana wao, yaani Ahazia na Yoramu (2Fal 1:1-8:15). Ulienea hata katika Yuda wakati wa utawala wa mwana wa Yehoshafati, Yehoramu, aliyemwoa Athalia binti wa Ahabu na Yezebeli (21:1-20; taz. maelezo ya 2Fal 8:16-24).

Mfalme aliyefuata katika Yuda, Ahazia, hali akiongozwa na mama yake Athalia na jamaa zake wa kaskazini, alishirikiana na ufalme wa kaskazini ulioabudu miungu, na hivyo hakuishi sana, ball alikufa angali na umri mdogo tu (22:1-9; taz. maelezo ya 2Fal 8:25-29; 9:21-29; 10:12-14). Wafalme wa Yuda na Israeli wote waliuawa na Yehu ambaye mapinduzi yake ya kushinda Ubaali katika ufalme wa kaskazini yameelezwa katika 2Fal 9:1-10:36.

Baada ya kifo cha mfalme wa Yuda, Athalia alijitwalia kiti cha enzi mwenyewe. Alitawala kwa muda wa miaka sita, na wakati huo alifanya yote aliyoweza ili kuimarisha Ubaali wa kaskazini wa wazazi wake katika Yuda. Lakini makuhani na Walawi waliendelea kuwa waaminifu kwa BWANA. Walawi hao walikuwa walinzi wa hekalu, na mwandishi alisisitiza kazi yao ya maana sana (pamoja na ile ya walinzi wa nyumba ya mfalme) ya kumwondoa Athalia na kurudisha kiti cha enzi katika ufalme wa nyumba ya Daudi. Pia mwandishi alionyesha kwamba, ingawa mapinduzi yalitokea katika uwanja wa hekalu, hakuna mtu aliyeingia hekaluni isipokuwa makuhani na Walawi. Watu walipaswa kuheshimu utakatifu wa hekalu (22:10-23:21; taz. maelezo ya 2Fal 11:1-20). Kifo cha Athalia kilileta mwisho wa Ubaali wa Yezebeli katika Yuda'.

Yoashi na Yehoyada (24:1-27) Utawala wa mfalme mpya Yoashi unaonyesha jinsi ukuhani wenye nguvu na uchaji wa Mungu ulivyotakiwa sana, ili wafalme wa mbari ya Daudi waweze kutimiza makusudi ya ufalme huo. Muda wote ambao Yoashi alikuwa chini ya uongozi na ushawishi wa kuhani mkuu Yehoyada, alikuwa mwaminifu kwa Mungu naye alihamasisha ibada ya kweli kwa watu wote. Baada ya kufa kwa Yehoyada, Yoashi alimwacha BWANA, akakaribisha ibada ya Kikanaani na kuwapinga manabii wa Mungu. Kwa sababu ya mambo hayo hukumu ya Mungu ilikuja juu yake. Hata kifo chake kilikuwa adhabu, kwa sababu alikuwa amemwua kuhani aliyethubutu kumkemea (24:1-27; taz. maelezo ya 2Fal 12:1-21).

Misiba inafuata mafanikio (25:1-28:27)

Kuhusu wafalme wa Israeli waliofuata, mwandishi wa Mambo ya Nyakati hakuandika neno (2Fal 13:1-25). Yuda haikutakiwa kuwa na uhusiano wo wote na ufalme wa kaskazini, wala isikodi askari wa Israeli. Ahazia wa Yuda alikubali ushauri huo, akapata thawabu ya ushindi mkubwa juu ya Waedomu. Lakini ushindi huo, badala ya kuongeza imani yake ya kumtegemea Mungu, ulimpa mawazo ya kiburi na uhuru wa binafsi yake. Alimwasi BWANA na kuabudu miungu. Hatimaye ufalme wa kaskazini usiomjali Mungu ulikuwa chombo cha Mungu cha kuadhibu ufalme wa kusini ulioasi (25:1-28; taz. maelezo ya 2Fal 14:1-22).

Chini ya utawala wa Yeroboamu wa pili wa kaskazini (2Fal 14:23-29) na wa Uzia (au Azaria) wa kusini, falme zote mbili zilikuwa na muda wa mafanikio na kupanuka. Kwa bahati mbaya, nguvu ya Yuda ilimvimbisha kichwa Uzia, na kwa kiburi chake alijitwalia haki ya kufanya kazi ya ukuhani. Mwandishi alionyesha wazi kwamba, ingawa huduma za ukuhani na ufalme zilipangwa na Mungu na zilitakiwa kufanye kazi pamoja, zilikuwa huduma tofauti, nazo zilitakiwa kutekelezwa na watu tofauti. Mtu mmqja hakuweza kufanya kazi ya mwingine (26:1-23; taz. maelezo ya2Fal 15:1-7).

Yothamu alifuata siasa njema ya baba yake, akijihadhari asije akarudia makosa yake. Mwandishi aliona kwamba ulikuwa uchaji wa Mungu wa Yothamu uliompa nguvu na mafanikio (27:1-9; taz. maelezo ya 2Fal 15:32-38).

Mafanikio makubwa katika falme zote mbili yalifuatwa na maafa makubwa yasiyoaminika. Ufalme wa kaskazini ulinusurika kuangamizwa (2FaI 15:8-31), na kusini utawala wa taabu kabisa wa Ahazi ulileta uharibifu mkubwa kwa Yuda, nusura kuangamia pia (28:1-27; taz. maelezo ya 2Fal 16:1-20). Mambo hayo yalitokea muda mfupi tu kabla ya ufalme wa kaskazini kuangamizwa kabisa na watu wake kupelekwa katika kifungo cha Uashuru. Utekaji ule ulikuwa mwisho wa ufalme wa kaskazini (2Fal 17:1-41).

Marekebisho ya dini chini ya Hezekia (29:1-31:21)

Mara baada ya kuwa mfalme, Hezekia alianza marekebisho makubwa ya dini ya Yuda, ambayo pia yalihamasishwa na mahubiri ya nabii Mika (Yer 26:17-19; taz. maelezo ya 2Fal 18:1-12). Mwandishi alieleza kirefu kazi mbalimbali za Hezekia, hasa sehemu zile zilizohusika na hekalu, makuhani na Walawi. Hezekia aliitisha mkutano wa makuhani na Walawi akawaambia wazi kwamba kudharauliwa kwa huduma ya hekalu kulimsababisha Mungu kukasirikia Yuda. Kazi yao ya kwanza ingekuwa kusafisha hekalu vizuri na kulikarabati ili liwekwe wakfu upya kwa ibada ya Mungu (29:1-11). Hekalu lilikuwa limechafuka sana, hata kundi kubwa la Walawi lilipaswa kushughulika zaidi ya majuma mawili ili kulisafisha na kuliandaa tena kwa matumizi (12-19).

Kisha Hezekia aliitisha ibada kubwa sana ambamo makuhani walitoa sadaka nyingi kwa ajili ya kutakasa na kuweka wakfu upya mfalme, taifa lote na hekalu (29:20-24). Mambo hayo yote yalipambwa na nyimbo nyingi za Walawi na muziki, kama ilivyopangwa na Daudi hapo awali (25-30).

Baada ya ibada, watu walikaribishwa kutoa sadaka zao binafsi. Waliitikia mara na kwa wingi kiasi kwamba makuhani hawakujiandaa kwa huduma hiyo, nao walishindwa kutimiza shughuli zote katika bidii mpya ya hekaluni. Walawi walioonyesha bidii zaidi, waliitwa ili wawasaidie makuhani (31-36).

Baada ya kuweka hekalu wakfu hivyo, Hezekia aliagiza sikukuu kubwa ya Pasaka. Marekebisho yake yalichelewa kuanzishwa ili Pasaka iadhimishwe katika mwezi wa kwanza wa mwaka (yaani muda uliopangwa katika sheria), hivyo iliahirishwa kwa mwezi mmoja (taz.Hes 9:10-11). Hezekia alialika Waisraeli wa kaskazini walioweza kuepukana na kupelekwa kifungoni, lakini wengi wao hawakupenda (30:1-12).

Wale waliokutana kwa sikukuu walisafisha Yerusalemu na kuondoa dalili zote za dini za kinyume. Bidii kubwa ya watu kwa usafi wa dini iliwahamasisha makuhani na Walawi wafanye haraka kujitakasa wenyewe kisheria kwa ajili ya sikukuu. Baadhi ya wageni waliochelewa kuwahi sherehe ya utakaso wa siku saba kabla ya sikukuu ya Pasaka, walishiriki sikukuu hiyo bila kutakaswa sawa sawa. Kutokana na maombi ya Hezekia, Mungu akawasamehe (13-22). Furaha ya sikukuu ikazidi sana, hata sikukuu yenyewe ikaongezwa muda wa juma moja zaidi (23-27).

Baada ya kumaliza kusafisha Yerusalemu na hekalu, watu walitoka nje na kusafisha nchi (31:1). Hivyo baada ya kuondoa dini za kinyume, Hezekia alifanya mikakati ya kuendesha dini ya kweli jinsi ilivyotakiwa. Kwanza, aliwagawa makuhani na Walawi katika makundi mbalimbali kadiri ya mipango ya kwanza ya Daudi (taz.lNya 23:1-26:32). Kisha alitimiza mipango ya posho zao kwa njia ya kuwahamasisha watu wote watoe zaka (yaani sehemu ya kumi ya mapato yote) na sadaka zao (2-7). Watu waliitikia kwa moyo sana, hata Hezekia akapaswa kuandaa nyumba na mazizi ya pekee kwa ajili

ya kondoo, ng'ombe na nafaka vilivyoletwa. Pia akaweka makarani waliotunza akiba hizo na kuandika orodha ya majina ya watu wote waliostahili kupata posho kutoka fungu hilo, ili mambo yote yaendeshwe kwa uaminifu bila wasiwasi (8-21).

Utawala wa kiraia wa Hezekia (32:1-33)

Kwa mwandishi wa Mambo ya Nyakati matengenezo ya kidini ya Hezekia yalikuwa mambo makuu kabisa ya utawala wake. Kwa upande wa siasa, Hezekia hakulazimishwa kuwategemea Waashuri, lakini hasa kwa sababu Mungu mwenyewe alijiingiza na kushughulika kama jibu la imani ya mfalme huyo (32:1-23; taz. maelezo ya 2Fal 18:13-19:37). Pia alileta mafanikio makubwa katika Yuda. Kwa bahati mbaya Hezekia alivimba kichwa kutokana na mambo yote aliyoweza kuyafanya na kupata, na kiburi hicho kilimsababisha afanye urafiki na Babeli, ufalme mpya ulioanza kupata nguvu katika maeneo ya mashariki. Siasa hiyo baadaye ilileta maafa na maangamizo juu yaYuda (24-33; taz. maelezo ya 2Fal 20:1-21).

Maovu ya Manase na Amoni (33:1-25) Manase anapata lawama zote za kuharibu kazi njema za baba yake na kwa kushusha taifa iote katika hali ya chini kabisa katika historia yake kuhusu mambo ya kiroho. Uharibifu aliouleta katika muda mrefu wa miaka 55 ya utawala wake, haukuweza kurekebishwa tena katika muda mfupi wa majaribio yake ya matengenezo karibu na mwisho wa maisha yake, wala haukuweza kurekebishwa na mfalme mwingine aliyetawala baada yake. Yuda ingepelekwa kifungoni kwa sababu ya uovu wake, kama ilivyokuwa kwa Israeli hapo awali (33:1-20; taz. maelezo ya 2Fal 21:1-18). Amoni aliyetawala miaka miwili tu aliondoa dalili zote zilizobaki za marekebisho ya baba yake (21-25; taz. maelezo ya 2Fal 21:19-26).

Marekebisho ya mwisho (34:1-35:27) Marekebisho mengine yalipita juu yaYuda wakati wa utawala wa Yosia (34:1-33; taz. maelezo ya 2Fal 22:1-23:20). Kama ilivyokuwa kwa Hezekia, machoni pa mwandishi kilele cha marekebisho yale kilikuwa sikukuu kubwa ya Pasaka Yerusalemu.

Baada ya kurudisha sanduku la agano mahali pa haki yake hekaluni, makuhani na Walawi walijiandaa kwa majukumu yao mengine. Yosia aliwapanga katika makundi mbalimbali, kama Hezekia alivyokuwa amefanya, kusudi mambo ya muziki, nyimbo, sadaka na sherehe nyingine ziweze kuendeshwa sawa sawa. Mfalme, majemadari wake na viongozi wa Walawi kwa ukarimu wao walitoa wanyama waliotakiwa kwa sadaka za watu wote kwa sikukuu hiyo. Sherehe yote ilikuwa kubwa kuliko ile ya Hezekia (35:1-19; taz. maelezo ya 2Fal 23:21-27). Inasikitisha kwamba Yosia aliuawa vitani alipokuwa na umri wa miaka 38 tu (20-27; taz. maelezo ya 2Fal 23:28-30).

Makosa, kushindwa na kifungo cha Babeli (36:1-23)

Mwandishi alieleza kwa kirefu marekebisho ya Hezekia na Yosia, akiwaonyesha wasomaji wake kwamba wafalme wema walijaribu kuwa waaminifu kwa sheria ya Musa na kwa maagano ya Daudi. Walipaswa kufuata kanuni za Kilawi kama walitaka kufurahia ahadi zilizotolewa kuhusu ufalme wa nasaba ya Daudi. Baada ya kifo chake Yosia, Yuda haikuchelewa kuzirudia njia zake za kumwasi Mungu. Wafalme waliofuata walikuwa na siasa ya hatari na uharibifu upande wa dini na siasa, na matokeo ya mambo yao yalikuwa hukumu ya mwisho ya Mungu juu ya taifa. Aliwaruhusu Wababeli kushinda Yuda, kubomoa Yerusalemu na kuwapeleka watu wake katika kifungo cha nchi ya kigeni.

Haikuwa makusudi ya mwandishi kueleza utekaji ule kinaganaga. Maelezo yale yaliandikwa katika Wafalme. Badala yake alisisitiza mambo yaliyosababisha kuangamizwa kwa Yuda, yaani kutoamini kwa makuhani na watu kwa jumla, na kukataa kwao maonyo ya wajumbe wa Mungu (36:1-21; taz. maelezo ya 2Fal 23:31-25:30).

Hata hivyo Mungu hakuwatupilia watu wake mbali. Miaka kama sabini baada ya mambo hayo, wakati mpya ulianza ambapo Koreshi, mfalme wa Uajemi, aliyekuwa ameshinda Babeli, alitangaza kwamba Wayahudi walikuwa hum kumdi katika nchi yao na kujenga taifa lao upya. Kama ilivyokuwa tangu awali, taifa hilo lilitakiwa kuweka hekalu la Yerusalemu liwe sehemu kuu ya maisha yake (22-23).

NYONGEZA ORODHA YA MAFUNGU YANAYOLINGANA

lNya	**1 Samweli**
-	1:1-30:31
1:1-9:44	-
10:1-14	31:1-13
	2 Samweli

-	1:1-4:12
11:1-9	5:1-10
11:10-47	23:8-39
12:1-40	-
13:1-14	6:1-11
14:1-17	5:11-25
15:1-16:3	6:12-23
16:4-43	-
17:1-27	7:1-29
18:1-17	8:1-18
-	9:1-13
19:1-19	10:1-19
20:1	11:1
-	11:2-12:25
20:2-3	12:26-31
	13:1-21:17
20:4-8	21:18-22
-	22:1-23:7
21:1-22:1	24:1-25
22:2-29:30	-
2Nya	**1 Wafalme**
-	1:1-3:3
1:1-13	3:4-15
-	3:16-4:34
1:14-17	10:26-29
2:1-18	5:1-18
3:1-5:1	6:1-7:51
5:2-7:22	8:1-9:9
8:1-18	9:10-28
9:1-28	10:1-25
-	11:1-40
9:29-31	11:41-43
10:1-11:4	12:1-24
-	12:25-14:20
11:5-12:16	14:21-31
13:1-22	15:1-8
14:1-16:14	15:9-24
-	15:25-21:29
17:1-19	-
18:1-34	22:1-40
19:1-20:30	-
20:31-37	22:41-50
-	22:51-53
	2 Wafalme
-	1:1-8:15
21:1-20	8:16-24
22:1-6	8:25-29
-	9:1-20
22:7-9	[9:21-29
	[10:12-14
-	9:30-10:11
-	10:15-36
22:10-23:21	11:1-20
24:1-27	11:21-12:21
-	13:1-25
25:1-26:2	14:1-22
-	14:23-29
26:3-23	15:1-7
-	15:8-31
27:1-9	15:32-38

28:1-27	16:1-20
-	17:1-41
-	18:1-12
29:1-31:21	-
32:1-33	18:13-20:21
33:1-25	21:1-26
34:1-33	22:1-23:20
35:1-27	23:1-30
36:1-21	23:31-25:30
36:22-23	